

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA**

**12 MEI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

**KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 12 MEI, 2026**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**307. MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO  
NDALICHAKO (KASULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya uhaba wa Watumishi wa Kada ya Afya katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu.

**308. MHESHIMIWA CHARLES MHANDO NJAMA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Vituo vya Afya Kata ya Old Korogwe, Kwamndolwa, Mtonga na Bagamoyo utaanza.

**309. MHESHIMIWA YOHANA STEPHEN MSITA (ITIGI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Kata za Mgandu, Mwamagembe, Ipole na Idonyandole Itigi.

**310. MHESHIMIWA HAIDERALI HUSSEIN GULAMALI (ILONGERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Soko la Vitunguu Njia panda ya Merya.

**311. MHESHIMIWA DKT. WILSON MAHERA CHARLES (BUTIAMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza na kukamilisha ujenzi na ukarabati wa Barabara katika Jimbo la Butiama.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**312. MHESHIMIWA SULEIMAN MOHAMED RADHID (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kero ngapi za Muungano zimetatuliwa mpaka sasa.

**WIZARA YA MAJI:**

**313. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa maji kwenye Mji Mdogo wa Kifanya katika Kata ya Kifanya.

**314. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mabwawa ya Maji ya Mihingo, Tingirima, Salama, Lakana, Kambubu na Nyaburundu.

**WIZARA YA NISHATI:**

**315. MHESHIMIWA HASNAIN GULAMABBAS DEWJI (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, mpaka sasa Visima vingapi vya Gesi Asilia vimechimbwa katika Kisiwa cha Songosongo na upi mpango wa kuongeza uzalishaji wa gesi.

**316. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini usambazaji wa gesi asilia majumbani katika Jimbo la Nanyamba utaanza.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **317. MHESHIMIWA MECKTRIDIS FRATERN MDAKU (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwaongezea maeneo ya Kilimo Wananchi wa Malinyi baada ya maeneo yao kuingizwa kwenye Hifadhi.

### **318. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaangalia upya gharama za uzalishaji wa Tumbaku ili Mkulima apate faida.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **319. MHESHIMIWA EDIBILY KAZALA KINYOMA (KASULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza mgogoro wa ardhi kati ya TFS na TAWA dhidi ya Wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **320. MHESHIMIWA THOMAS KAMPALA MAGANGA (KATAVI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami utanza kwa Barabara ya Inyonga - Majimoto hadi Kibaoni Km 162 kwa kuwa upembuzi yakinifu ulishakamilika.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **321. MHESHIMIWA MOHAMED MUSSA UTALY (LINDI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA AFYA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
12 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**